# DHAMBI NI NINI?

**Na Christopher Mwakabanje**

Biblia imeandikwa katika lugha tatu: Kiebrania, Kiarami na Kiyunani. Katika Agano Jipya neno dhambi limetafsiriwa kutoka neno la Kiyunani '*hamartia*' likimaanisha kukosea shabaha (missing the mark). Katika 1 Yohana 3:4, "*Kila atendaye dhambi afanya uasi; kwa kuwa dhambi ni uasi*." Uasi ni kuvuka mstari uliozuiliwa kuvuka. Dhambi imegawanyika katika mafungu mawili: (1) makatazo, na (2) kutotimiza wajibu. Kwa mfano: Usizini ni katazo; wakati upendo wa adui ni agizo la kutekeleza.

Katika Marko 10:19-22, tunasoma habari ya Mwanasheria Tajiri Kijana na kuona aina mbili za uvunjaji wa sheria. Aliweza kujizuia kutovunja karibu makatazo yote. Hakuwahi kuua, kuzini, kuiba, kushuhudia uongo, kudanganya, n.k. "*Akamwaambia, Mwalimu haya yote nimeyashika tangu utoto wangu. Yesu akamkazia macho, akampenda, akamwambia, umepungukiwa na neno moja. Enenda ukauze ulivyo navyo vyote, uwape maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni; kisha njoo unifuate.*" Agizo la kutimiza wajibu limetajwa moja tu, "waheshimu baba yako na mama yako," lakini amri zote katika fungu hilo ni makatazo.

Biblia pia inaelezea "*Kila lisilo la haki ni dhambi…*" (1 Yoh.5:17). Katika Kiyunani neno haki ni "*dikaiosune*" lenye maana ya tabia ya haki ya Mungu (Warumi 3:5); kama alivyo mwaminifu, mkweli, n.k. Watu wengi siku hizi huliangalia neno "haki" kwa mtazamo wa Umoja wa Mataifa (UNO). Lakini Biblia inasema, *"…Maana maagizo yako yote ni ya haki*" (Zaburi 119:172). Waisraeli walishutumiwa kwa kutafuta haki zao wenyewe. "*Kwa maana nawashuhudia kwamba wana juhudi kwa ajili ya Mungu, lakini si katika maarifa. Kwa maana, wakiwa hawaijui haki ya Mungu, na wakitaka kuithibitisha haki yao wenyewe, hawakujitia chini ya haki ya Mungu*" (Warumi 10:1-4). Ikiwa Mungu ndiye aliyetuumba, hivyo basi ana haki ya kutueleza jambo gani ni la haki na lipi si halali. "*Ole wao wasemao kwamba uovu ni wema, na kwamba wema ni uovu; watiao giza badala ya nuru, na nuru badala ya giza; watiao uchungu badala ya uchungu*!" (Isaya 5:20).

**JE, TUNAWEZA KURITHI DHAMBI?**

Tunarithi mali, nyumba, n.k. kutoka kwa wazazi, lakini si dhambi. Dhambi inakwenda na maneno KUTENDA au KUTOTENDA. Lazima mtu afikie umri wa kujua mema na mabaya. Katika Warumi 7:7 tunasoma, *"…Walakini singalitambua dhambi ila kwa sheria; kwa kuwa singalijua kutamani, kama torati isingalisema, Usitamani*." Watoto wadongo hawakuhusishwa katika uasi watu wazima Waisraeli. "*Tena wadogo wenu, mliosema watakuwa mateka, na wana wenu, wasio leo na maarifa ya mabaya wala mema, ndio watakaoingia, nao ndio nitakaowapa, nao wataimiliki*" (Kumb.1:39). Kwa kuwa watu wazima waliwaogopa wenyeji wa Kanaani (wasimwogope Mungu), Mungu aliwaangamiza wote jangwani kwa miaka 40, isipokuwa Kalebu na Yoshua. Neno la Mungu linasema, "*Na kama yeye* [**baba mwovu]** *akizaa mwana, naye* **[kijana]** *ameona dhambi zote za baba yake alizozitenda, akaogopa, asifanye neno lolote kama hayo…hatakufa huyo* **[kijana]** *kwa ajili ya uovu wa baba yake, hakika ataishi*" (Ezekieli 18:14-17). Katika mstari 20 tunasoma, "*Roho itendayo dhambi, ndiyo itakayokufa; mwana hatauchukua uovu wa baba yake, wala baba hatauchukua uovu wa mwanawe, haki yake mwenye haki itakuwa juu yake, uovu wake mwenye uovu utakuwa juu yake.*"

**MADHARA YA DHAMBI**

Dhambi ina madhara (consequence) makubwa sana! Ndiyo maana Mungu anatusihi sana tusitende dhambi. Dhambi humwaathiri mtendaji kadhalika watu wengine ambao hawajaitenda dhambi kama hiyo. Kwa mfano dhambi ya Adamu na Hawa, Biblia inasema, "*Kwa hiyo, kama kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, na kwa dhambi hiyo* ***mauti****; na hivyo mauti ikawafikia watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi; maana kabla ya sheria dhambi ilikuwamo ulimwenguni, lakini dhambi haihesabiwi isipokuwapo sheria; walakini mauti ilitawala tangu Adamu mpaka Musa, nayo iliwatawala hata wao wasiofanya dhambi ifananayo na kosa la Adamu, iliyo mfano wake yeye atakayekuja*" (Rum.5:12-14).

Katika fungu hilo hapo juu tunaona ni 'mauti' iliyowafikia watu wote. Tunakufa ikiwa ni athari za kosa la Adamu. Kuwa na HATIA (guilt) na kupata MADHARA ni mambo mawili tofauti. Watu wote **wamefanya** dhambi, Biblia haifundishi kwamba watu wote **wamerithi** dhambi. Ili mtu avunje sheria ni lazima pawe na sheria, kadhalika mtu huyo awe katika umri ambao atawajibika (accountable).

Hapa nitatoa mifano kubainisha tofauti: Mume aliyeoa halafu akatoka nje ya ndoa na kuambukizwa virusi vya ukimwi. Kisha akamwambukiza mkewe. Mkewe pia akachukua mimba na kumwambukiza mtoto aliyezaliwa. Mume, mke na mtoto wote wakafa, je! Mungu atawahukumu wote hao watatu kwa uzinzi? La! Hasha! Kila mtu atachukua furushi lake mwenyewe (Wagalatia 6:7). Mwenye hatia ni mume, lakini hao wengine wameathirika kwa matokeo ya dhambi ya mtu huyo mmoja. Tunakufa si kwa sababu tumerithi dhambi ya Adamu, bali kutokana na madhara ya dhambi hiyo. Hatuwezi kuupata mti ule wa uzima pale Bustanini Edeni. Ingekuwa kifo ni ishara ya kuonyesha kwamba mtu ni mwenye dhambi, basi unapaswa kukumbuka kwamba hata Yesu asiye na dhambi alikufa! (Ebr.4:15).

Mfano mwingine, kiongozi wa serikali fulani ameamua kula rushwa hata Hospitali za umma kukosa dawa. Unadhani watu wangapi watakufa kutokana na kukosekana kwa dawa katika hospitali husika? Wengi! Je, wote waliofikwa na mauti kutokana na kukosa matibabu ni wala rushwa? Jambo ovu tunalolitenda huathiri watoto wetu hata vizazi vingi (Kut.20:4-6).

" *Tazama, mimi naliumbwa katika hali ya uovu; mama yangu alichukua mimba hatiani*" (Zab.51:5). Fungu hili linatumiwa vibaya sana na watu wanaofundisha kwamba watoto wanazaliwa dhambini. Utata wa sentensi ya kwanza hujibiwa na sehemu ya pili ya fungu hilo "*Mama yangu alichukua mimba hatiani*." Hilo ndilo Daudi analolizungumzia. Mama yake alichukua mimba katika uzinzi. Watoa maoni wengi wanasema kwamba hapo anazungumzia ukoo wake ulitokana na zinaa ukiangalia Mwanzo 38:15-30. Yuda alizini na mkwewe Tamari aliyemzaa Peresi. Kuna vizazi kumi kutoka Peresi hadi Daudi. Mwana haramu hakuruhusiwa kuingia katika kusanyiko la Bwana (Kumb.23:2). Ndiyo maana tunasoma Daudi akisema, "Nalifurahia nilipoambiwa, na twende nyumbani kwa Bwana" (Zab.122:1). Katika ukoo huo Daudi ndiye uzao wa kumi (Angalia Mathayo 1:3-6).

Ukoo wa Daudi uliathiriwa na dhambi ya Yuda, lakini Mungu asingewahukumu kwa dhambi hiyo. Hata serikali zetu haziwezi kumfunga mtoto kutokana na hatia ya mzazi wake, ingawa mtoto ataathirika ikiwa mzazi atafungwa gerezani. Mtoto atakosa huduma za mzazi wake alizokuwa akipewa alipokuwepo. Kuwa na hatia na madhara yatokanyo na dhambi ni vitu

viwili tofauti kabisa. Mungu mwenye haki kuliko serikali dhalimu za duniani hawezi kamwe kumhesabia mtu hatia kutokana na makosa ya wazazi wake.

Mungu amemwuumba mwanadamu mnyofu, lakini mwanadamu amejivumbulia mavumbuzi mengi (Mhubiri 7:29). Biblia inasema dhambi huonekana katika mwanadamu katika ujana wake (Mwanzo 8:21). Kama watoto wangekuwa na dhambi Mungu asingelisema tufanane nao (1 Kor.14:20; Mt.18:2-4, n.k.).

Asante: Christopher Mwakabanje
kapalapala@yahoo.com

www.kanisalakristo.com